WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI HEMBETI,
S.L.P 187,
TURIANI.
.............................................

Kumb Na; HSS/.I/VOL.1/04
Ndugu.........................................
S/Msingi.....................................

YAH: TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Uongozi wa shule ya Sekondari Hembeti wanayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.

Hongera sana, unatakiwa kufika shuleni tarehe 04/01/2021 tayari kwa kuanza masomo na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2021.

YAFUATAYO NI MAAGIZO MUHIMU PINDI UNARIPOTI SHULE.

1. SARE ZA SHULE
   i. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.
   ii. Suruali kwa wavulana na sketi kwa wasichana za rangi ya kijani, sketi zishonwe kwa heshima zivuke magoti na mshono ni linda boksi sita na suruali zishonwe kiheshima zenye rinda mbili, mitindo ya jinsi HAITAKIWI.
   iii. Viatu vya ngozi vyeusi visivyo na visigino virefu wala kuchongoka na vyenye Kamba.
   iv. Soksi nyeupe jozi mbili(2) na begi la kubebea daftari.
   v. Sare za michezo /kazi za mikono.
      - Track suti nyeusi kwa wavulana na sketi ndefu nyeusi wasichana.
      - Tisheti au fulana moja ya blue.
      - Raba nyeusi jozi moja(1)
   vi. Hijabu ifanane na sare za shule, suruali pana na shati la mikono mirefu lifike magotini.
   vii. Sweta la kijani kwa wenye matatizo.

MKUU WA SHULE
HEMBETI SHULE YA SEKONDARI
S.L.P 187
TURIANI.

4. FOMU YA MZAZI/MLEZI

YAH: KUKUBALIANA NA KANUNI NA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Mimi………………………………………………………………………………………ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………………ninakiri kukubaliana na sheria/kanuni za shule pindi mtoto wangu afikapo shuleni na maelezo mengine ya shule yaliyoambatanishwa na yatakayotolewa na uongozi wa shule , kwani natambua kutofanya hivyo mwanafunzi huyo hatapokelewa shuleni kabisa.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………Tarehe………………………………

5. FOMU YA MKATABA /KIAPO CHA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO/FUJO/UCHOCHEZI NA MAKOSA YA JINAI

   Mimi……………………………………………………………………ambaye ni mwanafunzi Wa shule ya sekondari Hembeti nimesoma na kuelewa sheria na kanuni zote za shule, ninakiri na kukubaliana na kuahidi kwamba nitazingatia na sitoshiriki katika aina yoyote ya migomo, fujo, uchochezi na makosa ya jinai na endapo nitakiuka nichukuliwe hatua KALI kwa mujibu wa SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE zilivyotolewa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978.

   Sahihi ya mwanafunzi……………………………………………Tarehe………………..

   Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………………Tarehe……………………

6. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

MKUU WA SHULE
HEMBETI SHULE YA SEKONDARI
S.L.P 187
TURIANI.



Scanned with CamScanner

2. VIFAA VYA DARASANI NA NJE
   i. Daftari kubwa zisizopungua kumi (10), mathematical set, rula, kalamu ya wino wa blue au nyeusi na penseli.
   ii. Kila mtoto aje na Dictionary(Kamusi) ya English to English(Oxford) kwa matumizi yake.
   iii. Wavulana waje na reki moja iliyo imara.
   iv. Wasichana waje na kwanja na doo ndogo ya lita 10.

3. MAAGIZO MENGINE
   i. Kila mwanafunzi anatakiwa aje na picha mbili za pasipoti kwa ajili ya kubandika kwenye kadi zao za maendeleo.
   ii. Sheria na kanuni za shule zimeambatanishwa kwenye fomu hii.
   iii. Nenda kwa daktari wa serikali ukapimwe na akujazie fomu. Fomu hiyo utakabidhi kwa mkuu wa shule au makamu wa mkuu wa shule mara utakaporipoti.
   iv. Mzazi atapelekewa ripoti ya maendeleo ya mtoto wake kwani pamoja na kugharamia (elimu) kwa fedha nyingi pia husaidia katika kuboresha maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma.

"Mzazi mpende mwanao kwa kumpa mahitaji yake muhimu na kwa wakati"

KARIBU SANA HEMBETI SEKONDARI

..............................................

Shida Samueli Lukali

Mkuu wa shule.

MKUU WA SHULE
HEMBETI SHULE YA SEKONDARI
S.L.P 187
TURIANI.



Scanned with CamScanner

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu yam waka 1978, aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayomara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi, wafanya kazi wote , wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule ni muhimu.
(c) KUWAHI katika kila shuhguli za shule na nyinginezo utakazopangiwa.
(d) Kufahamu MIPAKA YA SHULE na KUZINGATIA KIKAMILIFU maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo nyakati zote za uwanafunzi wako katika shule hii.
(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(f) Kuvaa sare wakati unapotakiwa.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(h) Kutoongezea mapambo yoyote katika sare ya shule.
(i) Kutovaa mapambo ya mwili kama Hereni, Cheni, Bangili, Pete nk.

7. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi wa aina zote.
2. Ushoga na uasherati,kuvunja, kugombanisha ndoa za watu mitaani.
3. Ubakaji.
4. Ulevi wa matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, pombe za aina yoyote n.k
5. Kupigana na kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali za shule.
7. Kudharau bendera ya taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata mimba, kuharibu mimba, ndani nan je ya shule.
10. Kutoa au kushawishi mimba.
11. Kugoma, kuchochea au kuongoza au kuvuruga AMANI na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi/kumgomea mwalimu.
13. Kumiliki au kutumia simu ya mkononi.
14. Kuwekwa au kushiriki shughuli zote ukeketaji(kuchezwa)
15. Utoro sugu
16. Kubainika au kukutwa kwenye nyumba za starehe(kumbi za starehe)



MKUU WA SHULE
HEMBETI SHULE YA SEKONDARI
S.L.P 187
TURIANI.

Scanned with CamScanner

8. MEDICAL CERTIFICATE EXAMINATION
(To be completed by medical officer in respect of FORM I-IV)

Pupil full name……………………………………………………………………………………
Age:………………………………………………………………………………(Year)
Blood count (Red and shits)…………………………………………………………………
Stool Examinatiom……………………………………………………………………………
Urinalysis……………………………………………………………………………………
Syphilis Test…………………………………………………………………………………
Eye Test……………………………………………………………………………………
T.B Test……………………………………………………………………………………
Ears……………………………………………………………………………………
Chest……………………………………………………………………………………
Spleen……………………………………………………………………………………
Abdomen……………………………………………………………………………………

ADDITION INFORMATION: Age physical defect or impairment infections, chronic or family diseases etc.

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit /until for medical admission into boarding secondary School.

Signature……………………………………………………………………………………
Designation……………………………………………………………………………………



Scanned with CamScanner